Kwanza kabisa nikupongeze kwa uamuzi wa faida na wathamani sana wa kutaka kuanza kuandika kitabu, naamini huta ishia kuandika kutabu kimoja tu, natumaini siku za mbeleni utaandika vitabu vingi zaidi.

Kwanza nikutoe hofu kwamba hakuna aliye zaliwa anajua kuandika, wote unaoona wananaandika na wananitwa waandishi mashuhuri na wao walijifunza ujuzi wa kuandika.

Uandishi ni ujuzi na kama ni ujuzi basi unaweza kujifunza na wewe ukaupata. Uandishi wa vitabu ni ufundi wa kuyatumia maneno kufikisha ujumbe ulio ukusudia kwa watu husika. Ingawa siku za leo kuna vitabu sauti ambavyo ni matokeo ya vitabu maandishi( vitabu sauti ni vitabu ambavyo huna haja ya kusoma vyenyewe unasikiliza tu kuna mtu anakusomea kwa niaba yako hivyo badala ya macho kupita kwenye maneno masikio yanahusika zaidi)

Kwa maelezo hayo hapo juu, juu ya uandishi ninapata hitimisho kuwa mtu yeyote anayeamua kujifunza kuhusu ujuzi wa kuandika vitabu, basi tayari ana mwanzo mzuri wa safari yake ya kuwa mwandishi mashuhuri wa vitabu.

# Nikukaribishe ujifunze pamoja.

Emmanuel Minga.

# KWANINI UANDIKE KITABU

Naamini unapoanza safari ni muhimu ukajua sababu ya safari yako, hii itakusaidia pale utakapo pata changamoto njiani ujue nini cha kufanya.

Unajua  ni ngumu kukata tamaa njiani kama ukiijua sababu madhubuti ya wewe kuanza safari hiyo,  hivyo utakapotaka kukata tamaa utakumbua sababu ya kwanini ulianza, na sababu hiyo ndiyo itakutia nguvu ya kuendelee mbele.

Baba yangu aliniambia kwa mfano huu; kwamba endapo ninahitaji nyama au mayai, ninakuwa nina machaguo mawili

I. Kufuga kuku ili nipate nyama na mayai,
II. Nikanunue mayai na nyama sokoni

Unapofanya uchaguzi mmoja wapo ni muhimu ukajiridhisha vya kutosha kwamba maamuzi uliyo yachukua ni sahihi na hutoyajutia mbele ya safari.

Hivyo hata ikatokea umekutana na changamoto yoyote njiani utakuwa tayari unasababu ya msingi ya kukufanya usonge mbele na usiishie njiani.

Nimekuandalia sababu zifuatazo, za kwanini ninatamani na wewe uwe miongoni mwa wandishi na uandike kitabu.

Chagua sababu zitakazokufaa na zitakazokutia moyo wakati wowote utakapopitia changamoto.

Kuna wakati unaweza kukosa hamu ya kuandika, kama ukiijua sababu hutokata tamaa, kuna wakati hutajua uandike kuhusu nini? Lakini usikate tamaa endelea kujikaza, nitakuandikia pia siraha za kukusaidia unapokutana na changamoto mbali mbali kwenye uandishi.

Usijali nakuhakikishia utakuwa moja ya waandishi walio bora zaidi na wenye kutegemewa na jamii ili jamii ipate mwelekeo kupitia wewe (endapo huta kata tamaa).

Haya twende kwenye sababu ambazo nahitaji uzijue za kwanini unapaswa uandike kitabu, na huwenda si vitabu tu kuna uandishi wa makala kwenye magazeti, mitandaoni n.k.

1. kuna hazina ya maarifa ya kipekee upo nayo, na wewe ukishindwa kuitoa hakuna mtu mwingine anaweza akafanya hivyo badala yako.

   Kuna taarifa na uwezo wa uwasilishaji wa taarifa wewe unao ambao hakuna mtu mwingine anaweza kuufanya badala yako, yaani namaanisha ni wewe pekee ndiye unaweza kuuelezea.

   Sasa wewe usipofanya maana yake umeukosesha ulimwengu kitu cha kipekee sana ulichotakiwa kupokea kutokea kwako.

   Mfano kwenye tasnia ya vichekesho kuna mtu anaitwa brother k na mwingine anaitwa Joti (nimewatumia hawa kwa sababu wanafahamika sana)

   Hawa wawili wote wanafanya uchekeshaji, lakini ufundi wa joti kuchekesha ni tofauti na ufundi wa Brother K. unajua ni kwanini na huku wote wanafanya kitu kimoja? Ni kwa sababu kila mmoja na upekee wake.

Hata kwenye uandishi ni vivyo hivyo, kila mtu anaupekee wake na mwandiko wake usiofanana na mtu awaye yeyote.

Kitu kimoja kinaweza kuandikwa na waandishi wawili kwa lengo moja lakini radha zikawa tofauti. Ni sawa na wimbo unaimba alafu wengine wanakuja kutengeneza remix , wimbo unaweza kuwa ule ule ila kwa ufundi tofauti.

Hii ndiyo sababu natamani nawewe uandike kitabu ili ulimwengu upate radha nyingine kupitia karamu yako.

2. kuna watu usio wajua unapaswa uwaonyeshe njia, na usipofanya hivyo kuna sehemu utakuwa umewakatili na wewe utakosa baraka yako.

   Uandishi ni huduma kama huduma zingine za muhimu katika jamii.

   Hii ni kwa sababu ni huduma inayohusika kutatua matatizo katika jamii. Kwa maana hii ninaujasiri kukwambia jamii yako inamatatizo au

changamoto nyingi na baadhi yake zinakusubili wewe uandike ili zikatatuliwe kupitia ujuzi wako.

Usipo andika huwenda kuna watu watateseka na matatizo yao hadi kaburini, unapaswa kuandika, hicho unachokiona ni kidogo hivyo hivyo na udogo wake kuna mtu anahitaji msaada huo.

Kuna shuhuda watu utawasikia wakisema, nilidhamilia kujidhuru lakini niliposoma kitabu chako nikapata ukombozi, au mtu anasema niliposoma kitabu chako nilipata wazo ambalo lilinifanya niweze kufanya mambo makubwa, kama vile kuna wafanya biashara wakubwa walianza biashara kwa sababu walihamasishwa na mwandishi fulani.

Andika kuna watu watakutazama ili wapate kufanya maamuzi thabiti kwa maisha yao. wewe huwajui lakini Mungu anawajua. Andika uwasaidie wengine wanaohitaji msaada wako pasipo wewe kuwajua.

3. kuna watu wamebeba fedha zako na huwezi kuzipata hadi siku utakapowapa zawadi ya maarifa utakayo yaandika kitabuni.

Kuna mamilioni ya fedha yamejificha kwenye kurasa za vitabu ambazo hujaziandika.

Kwa kuandika unaweza kuwa tajiri na mtu mwenye mafanikio makubwa ikiwa tu utamaanisha.

Watu wanazo fedha kwa ajili yako, lakini hawawezi kukupa ukiwa mikono mitupu ,ni sharti uwape thamani fulani wanayoihitaji ndipo wakupe hizo fedha.

Ukiandika dawa ya matatizo ya watu watu watakuja kununua kitabu chako ili wapate majibu ya uhitaji wao.

Watu huwekeza sehemu wanayoona inawanufaisha, na hivyo hapa ninakupa siri nyingine ya mafanikio kwenye uandishi, andika dawa ya tatizo linalosumbua watu wengi zaidi,

kwa sababu kwa kadri ya watu wengi wanavyohitaji utatuzi wa shida zao itawabidi watafute kitabu chako na wanunue.

Kama ilivyo hospitali, ambavyo ni kimbilio la wagonjwa kila siku, vivyo hivyo na kitabu chako kinapaswa kiwe kimbilio la wahitaji wengi wanaohitaji elimu uliyoiandika humo itakayotatua matatizo yao.

Uandishi ni mgodi wa fedha ambao hata vizazi vyako vitafaidi urithi wake.

Marehemu dr.Myles Munroe alifariki mwaka 2014, huyu ni moja ya waandishi nguli walioandika sana kwa habari ya uongozi, maendeleo binafsi na mahusiano, aliandika zaidi ya vitabu sitini na sita(66) alifaidi uwekezaji wake na hadi leo watoto wake na wajukuu zake wanafaidi hazina ya fedha za mauzo ya vitabu vyake.

Ukiandika kitabu utauza hadi unakwenda kaburini na vizazi baada yako nao watafaidi pia. Andika huu ni urithi wa vizazi vyako.